

MATUMAINI PROG NO:2523

TITLE: THE SOCIETY OF THE FAITHFUL.

SUMMERY: KINATUHIMIZA KUHUSIANA NA KUTENDA MEMA NA KUSHIRIKIANA KAMA WAKRISTO.

TEXT: WAEBRANIA 13:10-16.

MADA: JAMII YA WAAMINI.

.....
Kabla ya kuendelea na somo hili la leo,,hebu kwanza kabisa tukapate kumshukuru Mungu kwa nafasi hii.
Natuombe;

OMBI.... Mungu Mkuu na tena Mshahuri wa ajabu uliyetuumba,,,; tunakushukuru kwa sababu ya ulinzi na zaidi mno uwepo wako pamoja nasi hadi kwa sasa hivi. Tunapolianza somo hili la leo kuhusiana na Jamii ya waamini ,,fungua mioyo yetu ili tukaweze kulielewa vyema. Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Mpendwa,,ni fursa nyingine ya kufurahia maana Mungu wetu ametujalia tena nafasi ya kujifunza kutoka Nenoni mwake. Ninayo imani ya kwamba,, unaendelea vyema.

Karibu sana ili tukaweze kujifunza Neno lake Mwenyenyezi Mungu kuhusiana na *Jamii ya waamini* .

Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.

Somo ni kutoka kwenye Waebrania 13:10-16.

Kwa hitimisha fundisho leo,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo huu

WIMBO:

Ni kweli kabisa ya kwamba Mungu ni Bwana wa wote wenye mwili,,Asante sana mtumishi Eunice Ferdinand kwa wimbo huo kwa jina mzuri sana yaani Twakumini Yesu.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Rafiki yangu,,,kila kundi humu ulimwenguni,,bila shaka linayo masharti au kwa lugha nyingine kanuni zake. Mataifa yana sheria zao, mashirika yana miongozo yao, na hata familia huwa na taratibu zinazowaongoza.

Vivyo hivyo, Mungu wetu anao watu wake wanaoitwa waamini. Hawa ni wale waliookolewa kwa imani katika Yesu Kristo na kuwa sehemu ya familia ya Mungu.

Mpendwa,,,swali kuu ni hili,,,Je!,,Mtu anaingiaje katika jumuiya ya waamini?

Tunapolichambua neno kutoka kwenye Waraka huu kwa Waebrania 13:10-16,,,tunayapata masharti muhimu yanayotuongoza katika suala hili.

Fungu hili la neno linasomeka hivi;

10. Sisi tunayo madhabahu, ambayo wale wanaoitumikia hema hawana haki ya kula vitu hivyo.

11. Kwa maana miili ya wale wanyama ambao damu yao huletwa ndani ya Patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, miili yao huchomwa nje ya kambi.

12. Kwa hiyo Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.

13. Basi na tumwendee nje ya kambi, tukiichukua aibu yake.

14. Kwa maana hapa hatuna mji udumuo, bali twatafuta ule ujao.

15. Basi kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake.

16. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana;

.....

Msikilizaji wangu,,kama ambavyo tumelishiriki neno hili,,,tunapata kuliona Sharti la kwanza kabisa ambalo ni kuhusiana na,,,Huduma ya Kipekee.

Katika aya ya 10,,,Biblia inasema ya kwamba;"Sisi tunayo madhabahu, ambayo wale wanaoitumikia hema hawana haki ya kula vitu hivyo."

Katika Agano la Kale, Mungu aliwaamuru wana wa-Waisraeli kutoa sadaka za dhambi. Sadaka hizo zilitolewa na kuhani mkuu katika madhabahu maalum.

Ndugu pamoja na dadangu,,,mnyama aliyetolewa kama sadaka,,neni linatuambia kuwa,,,alichinjwa kwa ajili ya dhambi za watu, na mwili wake kuchomwa nje ya kambi.

Hii ilikuwa picha ya jambo kubwa ambalo lingekuja kutimizwa na Yesu Kristo.

Sadaka zote za Agano la Kale zilikuwa zikimwelekeza mwanadamu kwa Mwokozi ambaye angekuja kuondoa dhambi za ulimwengu.

Kwa hiyo, huduma hiyo ya kipekee ilikuwa maandalizi ya kazi kuu ya Yesu Kristo.

Sharti la pili rafiki yangu,,,ni kuhusiana na,,,mateso ya Kipekee ya Yesu.

Aya ya 12 inasema; "Kwa hiyo Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango."

Yesu Kristo ndiye sadaka kamili kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote.

Bwana wetu Yesu Kristo,,Alisulubishwa nje ya mji wa Yerusalemu na kumwaga damu yake kwa ajili yetu.

Tofauti na sadaka za wanyama zilizotolewa mara kwa mara, Yesu alijitoa mara moja tu na sadaka yake ikatosha milele.

Biblia inasema katika 2 Wakorintho 5:21 kwamba;"Yeye asiyejua dhambi alifanywa kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."

Mpendwa Bwana wetu Yesu Kristo alibeba aibu, hukumu na adhabu iliyokuwa inatustahili sisi.

Kwa njia ya mateso yake tunapata msamaha wa dhambi na kuingia katika familia ya Mungu.

Msikilizaji mpendwa,,,hakuna mtu anayeweza kuwa sehemu ya jumuiya ya waamini bila ya kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wake....Na hili nakukuhakikishia.

Sharti la tatu na la mwisho kwa leo kutokana na fungu hili,,ni kuhusiana na,,
Dhabihu ya Kipekee.

Baada ya kuokolewa, Mungu anatarajia waamini wayaishi maisha ya kumshukuru na zaidi sana maisha ya kumwaabudu.

Biblia inasema hivi katika ya 15;"Basi kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima."

Mpendwa,,kwa sasa,,,sisi hatutoi tena sadaka za wanyama na badala yake, tunamtolea Mungu sifa,shukrani,ibada na zaidi mno kuyaishi maisha ya utiifu.

Dhabihu yetu ni matunda ya midomo yetu tunapolisifu jina la Bwana.

Lakini sifa za kweli lazima zionekane pia katika matendo yetu.

Ndiyo maana aya ya 16 katika Waraka huu kwa Waebrania 13,,Bibilia inaendelea na kusema hivi; "Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana."

Mkristo wa kweli humsifu Mungu kwa maneno yake na pia kwa maisha yake.

Anawasaidia wengine, anashirikiana nao, na anaonyesha upendo wa Kristo kwa vitendo.

Kwa kumalizia nataka tukakumbushane kwa mhtasari mafundisho 3 ambayo tumeyapata kwenye Waraka huu kwa Waebrania 13:10-16,,,,ili kuingia kwenye jamii ya waamini:

Kwanza kabisa ni kupitia kwa,,,huduma ya kipekee iliyoashiria wokovu unaokuja.

Pili ni kwa njia ya mateso ya kipekee ya Yesu Kristo aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Tatu na mwisho,,ni kupitia kwa dhabihu ya kipekee ya sifa, shukrani na matendo mema kwa Mungu.

Mtu anapomwamini Yesu Kristo na kuikubali kazi yake msalabani, huwa sehemu ya familia ya Mungu na kuingia katika jumuiya ya waamini.

Huo ndio msingi wa ushirika wa kweli pamoja na Mungu na watu wake.

Ningependa kukuacha na kifungu ambacho ni cha Kutia Moyo kutoka kwenye 1 Petro 2:9.

Kinasomeka hivi; "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili leo kuhusiana na njia za kufanyika kuwa katika jamii ya ya waamini. Tusaidie kupitia kwa Roho wako ili tukaweze kufanikiwa kupatikana katika jamii hiyo.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr Kenya.Leo mada yetu imekuwa ni;Jamii ya waamini.

Tumeutoa kwenye Waraka kwa Waebrania 13:10-16.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,barikiwa kupitia kwa wimbo huu,, ...

WIMBO.....

Ni wimbo Baba tunakuabudu na wana-Sounds of Afrika..

Asanteni sana waimbaji wetu kwa wimbo huo mzuri wa kuabudu.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri